



PENDEKEZO LA KUONGEZA BEI ZA HUDUMA YA UMEME KWA 40%

MABADILIKO YA UKUMBI KWA DAR ES SALAAM

MIKUTANO YA KUPATA MAONI KUHUSU MAOMBI YA SHIRIKA LA UMEME TANZANIA (TANESCO) YA KUONGEZA BEI ZA HUDUMA YA UMEME

MAHALI	TAREHE	MUDA	UKUMBI
MBEYA	19/11/2007	SAA 8 MCHANA	UKUMBI WA MKUTANO WA MKAPA
MWANZA	20/11/2007	SAA 8 MCHANA	MKUMBI WA MKUTANO WA MAHATMA GHADHI
ARUSHA	20/11/2007	SAA 8 MCHANA	UKUMBI WA MKUTANO WA BENKI KUU
DODOMA	21/11/2007	SAA 8 MCHANA	UKUMBI WA KILIMANI
DAR ES SALAAM	23/11/2007	SAA 4 ASUBUHI	UKUMBI WA MKUTANO WA KARIMJEE *

***Tafadhali zingatia mabadiliko ya ukumbi kwa Dar es Salaam, kuwa**

sasa utakuwa Karimjee badala ya Diamond Jublee kama ilivyotangazwa hapo awali.

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (yaani *The Energy and Water Utilities Regulatory Authority (EWURA)*), imepokea maombi ya **Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) yenye Kumbukumbu Nambari -TR-E-07-012** ya kutaka kuongeza bei (*tariff*) za huduma za kusambaza umeme kwa asilimia 40 (40%). Pia TANESCO wamewasilisha ombi la kuongeza gharama za kuunganisha umeme (*new service line charges*) kwa kati ya asilimia 196 na 280 (196% - 280%).

Kwa mujibu wa kifungu cha 19(2)(b) cha Sheria ya EWURA, EWURA itafanya mikutano (taftishi/uchunguzi) ya kupata maoni kutoka kwa wadau na mwombaji ili kujua uhalali wa maombi hayo ya kupandisha bei ya huduma za Umeme.

Mikutano hiyo itakayofanyika **Dar Es Salaam, Arusha, Mwanza, Dodoma na Mbeya**, ili kupata maoni ya wananchi, Baraza la wawakilishi wa watumiaji wa huduma za umeme (yaani *Consumer Consultative Council (C.C.C)*), **Government Consultative Council (G.C.C)**, pamoja na wadau wengine kuhusu ombi hilo la **TANESCO**. Wawakilishi wa **Menejimenti ya TANESCO** pia wamealikwa kwenye mikutano hiyo ili washiriki kwenye taftishi hii/uchunguzi huu. Tarehe za mikutano hiyo, muda na mahali itakapofanyika ni kama ilivvyoanishwa kwenye jedwali hapo juu.

Wadau wengine ambao wanapenda kutoa maoni kuhusiana na taftishi/uchunguzi huu wanakaribishwa kuleta maoni yao ki-maandishi na kuyafikisha kwenye anuani iliyoonyeshwa hapa chini, kabla ya siku ya **Alhamisi tarehe 6 Desemba, 2007**.

*Imetolewa na Mkurugenzi Mkuu,
Mamlaka ya Udhibiti wa huduma za Nishati na Maji (EWURA)
Ghorofa ya 6, Harbour View Towers (zamani JM Mall Building),
Barabara ya Samora Avenue,
P. O. Box 72175, DAR ES SALAAM
Tel: 022 2123850/3/4/6, Fax: 022 2123180,
e-mail:info@ewura.com*